## Maswali

1. Mbona Hamani alipanga kuua Wayahudi wote?
2. Mordekai aliuliza Esta afanye nini?
3. Mbona Esta aliogopa kwenda kwa Mfalme?
4. Esta na Wayahudi walifanya nini kwa siku tatu?
5. Mfalme alifanya nini Esta alipoenda kumwona?
6. Esta aliuliza wakina nani wakuje kwa karamu ya chakula cha jioni?
7. Hamani alifanya nini Mordekai alipokataa kumwinamia tena?
8. Mfalme alisoma nini kwa kitabu chake cha kumbukumbu?
9. Hamani alifanya nini kama shukrani kwa Mordekai?
10. Esta aliambia Mfalme nini walipokuwa kwa karamu ya chakula cha jioni?
11. Nini ilifanyika kwa Hamani?
12. Wayahudi walipona namna gani?

## Majibu

1. Alichukia Mordekai kwa sababu alikataa kumwinamia.
2. Mordekai alitaka Esta aende aambia Mfalme aokoe Wayahudi.
3. Hakuna aliyekubaliwa kumwona Mfalme mpaka awe ameitwa.
4. Esta na Wayahudi walifunga na kuomba.
5. Mfalme alinyosha fimbo yake ya dhahabu na Esta hakuawa.
6. Esta aliuliza Mfalme na Hamani wakuje kwa karamu yake ya chakula cha jioni.
7. Hamani alifanya miti kubwa ya kumnyongea Mordekai.
8. Mfalme alisoma kwamba Mordekai alikuwa ameokoa maisha yake.
9. Hamani alizunguka mji wote kwa farasi ya mfalme akiambia watu kwamba Mordekai alikuwa amemfurahisha Mfalme.
10. Hamani alikuwa amepanga kumuua yeye na Wayahudi wote.
11. Hamani alinyongewa kwa miti yenye alipanga Mordekai anyongewe.
12. Sheria ilitengenezwa ya kwamba Wayahudi waue maadui wao wote.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1    Mwaka wa 3**

# 35 Esta anaokoa watu wake

## Marejeo

Esta mlango wa 3: 1 – 6 & 6 – 17;
Esta mlango wa 6 na mlango wa 7: 1 – 6 & 9 – 10

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu husaidia wanaomwamini na walio na ujasiri wa kufanya yanayotakiwa. Mungu huadhibu waliowaovu.

## Maneno maalum

35.1 Hamani muovu + Mordekai + asimwinamie + chukia + shauri mbaya + ua Wayahudi wote + Mfalme + sheria

35.2 Mordekai + Esta + uliza mfalme + hakubaliwi + funga na kuomba + Esta mjasiri + Mfalme + nyosha fimbo ya dhahabu

35.3 Esta + chakula cha jioni + Hamani + Mordekai hakumwinamia + miti ya kunyongea

35.4 Mfalme + hakulala + kitabu cha kumbukumbu + Mordekai alimwokoa + zawadi + Hamani + mpe Mordekai zawadi

35.5 Esta + tafadhali okoa uhai wetu + Hamani muovu + miti ya kunyongea + sheria ingine + Wayahudi waue maadui + Mungu aliokoa

**35.1** Hamani muovu alimchukia Mordekai, Myahudi. Hamani alikuwa mtu wa maana sana na alifikiria kwamba kila mtu lazima amuinamia. Mordekai alipenda Mungu na hangeweza kuinamia mtu. Hili jambo lilimkasirisha Hamani sana. Hamani alimchukia Mordekai na alipanga kumuua. Hamani alijua Mordekai alikuwa Myahudi na alitaka kuua Wayahudi wote kwa nchi hiyo. Hamani alikuwa muovu sana. Hakujali watu wangapi watakufa bora yeye ameadhibu Mordekai.

Hamani aliuliza Mfalme aweke sheria ya kusema kwamba Wayahudi wa milki yake yote wauawe. Aliambia Mfalme Ahasuero kwamba Wayahudi hawakutii amri za mfalme. Hata alipea Mfalme pesa nyingi ili hiyo sheria ipitishwe. Kwa hivyo hiyo sheria ilipitishwa na kuweka mhuri wa pete ya mfalme ili isibadilishwe. Mfalme Ahasuero hakujua kwamba Esta alikuwa Myahudi.

**35.2** Wayahudi wote kwa hiyo nchi walitishika sana. Mordekai aliudhika sana hata na Malkia Esta. Mordekai aliuliza Esta aende kwa Mfalme ili Wayahudi wapone. Lakini mtu yeyote hakuruhusiwa kwenda kumwona Mfalme mpaka awe amemwita. Ukidhubutu kwenda kumwona bila kuitwa, utauawa - la sivyo, Mfalme akunyoshee fimbo yake ya dhahabu.

Wayahudi waliendelea kushurutisha Esta aende kuona Mfalme na afanye jambo juu ya hiyo sheria mpya mbaya. Esta na Wayahudi wote walifunga na kuomba Mungu kwa siku tatu. Halafu Esta akahatarisha maisha yake na akaenda kumwona Mfalme bila mfalme kutumanisha kwamba aende. Esta alipokuwa akienda, Mfalme alinyosha fimbo yake ya Dhahabu – hivyo alikuwa amepona!

**35.3** Esta alipiga magoti mbele ya Mfalme na akaguza juu ya fimbo ya dhahabu. Alimuuliza kwamba yeye na Hamani wakuje kwa karamu ya chakula cha jioni siku hiyo. Wakati wa hiyo karamu, Esta aliuliza Mfalme na Hamani wakuje tena kwa karamu ingine kesho yake. Hapo ndiyo angemwambia hicho kitu cha maana alichotaka kumwambia.

Hamani alijisikia sana. Alijisikia kwa sababu aliona kwamba Malkia amemheshimu kwa kumwita yeye na Mfalme kwa karamu ya chakula chake cha jioni mara mbili. Alipokuwa akirudi nyumbani kutoka kwa karamu, alimwona Mordekai, Myahudi. Mordekai alikataa kumwinamia.

Hamani alikasirika sana na akawa na mpango, akatengeneza miti kubwa ya kunyongea Mordekai. Aliienda asubuhi kwa jumba la mfalme ili aulize Mfalme kama anaweza kumnyonga Mordekai.

**35.4** Usiku huo Mfalme hakuweza kulala. Aliitisha wamletee vitabu vyake vya kumbukumbu na wamsomee. Mtumishi wake alimsomea vile Mordekai alikuwa ameokoa Mfalme asiuawe. Mfalme akakumbuka kwamba hakuwa amempa Mordekai zawadi ya kumshukuru kwa kuokoa maisha yake.

Asubuhi na mapema, Hamani alikuja kwa Mfalme. Mfalme alimuuliza, “Ni zawadi gani ninaweza kumpa mtu mwenye amenifanyia mazuri?” Hamani alikuwa mtu wa kujipenda. Alifikiria kwamba Mfalme alitaka kumfanyia yeye. Alijibu, “Huyo mtu avae nguo za Mfalme, azungushwe kwa mji wote kwa farasi ya Mfalme akiambia kila mtu kwamba hivi ndivyo Mfalme anaweza kushukuru mtu aliyemfanyia mazuri.” Hamani alishangaa na akawa na uoga Mfalme alipomwamrisha, “Enda na ufanyie Mordekai, Myahudi hivyo!!”

**35.5** Baadaye jioni, wakati wa karamu kwa chakula cha jioni, Esta aliambia Mfalme, “Mimi na watu wangu tunaenda kuuawa. Tafadhali okoa maisha yetu.” Mfalme alishangaa kusikia hayo na akauliza sababu yake. Esta alielezea Mfalme mpango wa Hamani kuua Wayahudi wote. Alimwambia kwamba yeye ni Myahudi. Mfalme alikasirika sana sana. Mtumishi wa Mfalme mmoja akamwambia kwamba Hamani ametengeneza miti ya kumnyongea Mordekai. Aliamrisha kwamba Hamani anyongewe kwa hiyo miti yenye alitengeneza.

Sheria yenye ilikuwa imetengenezwa haingebadilishwa. Mfalme aliamrisha Mordekai awe na amri ingine ya kuwaruhusu Wayahudi waue maadui waliotaka kuwaua. Wajumbe walitembeza hiyo amri mpya kwa milki yote. Siku ilipofika Wayahudi hawakuawa. Badala yake maadui wa Wayahudi waliuawa! Wayahudi ni watu wa Mungu na Mungu anawapenda. Kwa hivyo Mungu alifanya haya mambo yote yafanyike ili aokoa Wayahudi kutoka kwa mpango muovu wa Hamani.